

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA TARIME



31/07/2023

TANGAZO LA ZABUNI MARUDIO NA: LGA/067/2023-2024/S/01.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime anapenda kuwatangazia wananchi wote wenye sifa na uwezo kutoka ndani na nje ya Wilaya ya Tarime kwamba anakaribisha maombi kwa zabuni ya USAFI WA MAZINGIRA katika Halmashauri kwa mwaka wa fedha **2024/2024**

1. ZABUNI YA USAFI WA MAENEO KATIKA KATA ZIFUATAZO YAFUATAYO

Maelezo ya kazi	Namba ya zabuni
KATA YA MATONGO	LGA/067/2023/2024/S/01LOT 2
KATA YA NYAMWAGA	LGA/067/2023/2024/S/01LOT 3
KATA YA SIRARI	LGA/067/2023/2024/S/01LOT 4

a) SIFA NA MASHARTI YA MWOMBAJI:-

- i. Mwombaji awe raia wa Tanzania
- ii. Mwombaji anatakiwa kufanya utafiti kwenye eneo analotarajia kufanya usafi ambapo mزابuni atakuwa anakusanya, anazoa, atasafirisha na utupa taka katika eneo maalum
- iii. Mwombaji aambatanishe kivuli cha leseni hai ya kazi ya uzoaji taka
- iv. Mwombaji awe na hati ya usajili wa walipa kodi (TIN) pamoja na hati ya usajili iwapo mwombaji ni kikundi, Ushirika au Kampuni. Iwapo mwombaji ni mtu binafsi awe Raia

- wa Tanzania na aambatanishe barua ya utambulisho wake kutoka kwa Mwenyekiti wa Kitongoji na Kijiji pamoja na kivuli cha kitambulisho cha mkazi/ Mpiga kura
- v. Mwombaji awe na Uzoefu wa kazi aliyoomba kwa muda wa mwaka (1) katika kazi hiyo.
 - vi. Mwombaji awe na Uthibitisho wa ulipaji kodi (Tax clearance certificate)
 - vii. Mwombaji asiwe mtumishi au Kiongozi katika Halmashauri ya Wilaya ya TARIME.
 - viii. Uthibitisho wa uwezo wake kifedha (Bank statement) kuanzia Julai 2022 hadi Juni 2023.
 - ix. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of attorney) wa mtu atakayehusika na zabuni hii.
 - x. **Awe na wafanyakazi / vibarua wa kutosha (CV).**
 - xi. **Awe na wataalaam washauri wa fedha, Afya na mazingira**
 - xii. Mwombaji wa zabuni anapaswa kuambatanisha dhamana ya zabuni kwa ahadi [**Bid Security Declaration**]
 - xiii. Mwombaji awasilishe mpango kazi unaoonyesha jinsi atakavyotekeleza majukumu yake katika kipindi cha makatiba.
 - xiv. Mwombaji anatakiwa alipe ada ya maombi ya **Tshs. 20,000.00** ambayo haitarudishwa. Kwa kutumia Control No. ya Halmashauri.
 - xv. Mwombaji atapatiwa Nyaraka za **Zabuni kutoka Ofisi ya Katibu wa Bodi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tarime (ofisi ya zamani Bomani) baada ya kulipa ada ya maombi TSHS. 20,000/=**
 - xvi. Zabuni hii ipo wazi kwa mtu binafsi, kikundi cha watu kilichosajiliwa Kisheria, Ushirika, Kampuni au Serikali ya Kijiji, ilimradi awe na sifa na uwezo wa kufanya shughuli hizi na awe tayari kuheshimu Mkataba.
 - xvii. Mwombaji ambatanishe katika maombi yake tamko la kutojikusisha na vitendo vya Rushwa au ushawishi wa aina yoyote, fomu ya tamko hili imeambatanishwa ukurasa wa mwisho wa kitabu cha zabuni.


NB: Mwombaji anaruhusiwa kupata ufafanuzi wa sharti lolote asilolielewa kabla ya kutuma maombi yake.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI:

1. Maombi yatumwe kwa anuani ifuatayo.

Katibu Bodi ya Zabuni
Halmashauri ya Wilaya ya Tarime
S.L.P 16
TARIME.

2. Juu kabisa ya Bahasha paandikwe kwa herufi kubwa Zabuni ya usafi katika kata ya (Taja aina ya Zabuni) unayoomba na katika bahasha hiyo pasionyeshe alama yoyote ya utambulisho wa mwombaji juu ya bahasha pia paandikwe usifungue kabla ya saa **4.30 asubuhi**.
3. Bahasha ifungwe madhubuti kwa **LAKIRI** na ndani ya bahasha iambatanishwe stakabadhi halisi ya malipo ya ada ya maombi, na vivuli vya leseni, cheti cha usajili wa kampuni, cheti cha utambulisho wa kampuni kisheria (certificate of incorporation) na hati mbalimbali zenye kutambulisha uhalali wa mwombaji / maombi.
4. Nyaraka za maombi ya Zabuni ikiwa imeambatanishwa na barua ya maombi itumbukizwe ndani ya Sanduku la Zabuni lilipo katika Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W) (ofisi ya Halmashauri ya zamani Bomani) **kuanzia saa 2.00 asubuhi hadi saa 9.30 mchana siku za kazi tu**. Mwombaji anapaswa kusaini katika kitabu cha kupokelea zabuni
5. Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ni saa 4.00 kamili asubuhi siku ya **tarehe 07/08/2023**. Zabuni zitafunguliwa siku hiyo hiyo ya mwisho wa kupokea maombi.
6. Mwombaji /mwakilishi wake anashauriwa kuhudhuria zoezi la ufunguzi litakalofanyika kuanzia saa 4.30 asubuhi katika ukumbi mdogo wa Halmashauri ya Tarime (Ofisi ya Halmashauri - Bomani)
7. Zabuni inadumu (Tender validity) kwa muda wa siku 30 baada ya ufunguzi.
8. Maombi yaliyochelewa, ambayo hayakusomwa wakati wa ufunguzi au yaliyotumwa kwa Fax, Telex, Telegram au maombi yaliyonakilishwa hayatafikiriwa kwa namna yoyote ile.



Solomon .I. Shati

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
TARIME.